Jinsi Ya Kuwa Na Nguvu

(How To Remain Strong)

Na

Ellis P. Forsman

Jinsi Ya Kuwa Na Nguvu

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 12, 2011

Jinsi Ya Kuwa Na Nguvu

2 Kor. 4:16-18

2 Kor. 4:16-18, "*Kwa hiyo hatulegei; bali ijaapokuwa utu wetu wan je unachakaa, lakini utu wetu wa ndani utafanywa upya siku kwa siku. Maana dhiki yetu nyepesi iliyo ya muda wa kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana; tusiviangalie vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Kwa maana vinaavyoonekana ni vya muda tu; bali visivyoonekana ni vya milele.*"

Mapema katika kifungu hiki Paulo anaonyesha ni kwa nini aliteseka kwa ajili ya huduma ya Bwana, na kwa nini alikuwa jasiri.

Katika misitari hii Paulo anaonyesha ni kwa nini alikuwa na nguvu. Hii ni wazi kwa Mkristo leo.

Paulo, "alisema hatuzimii roho." Kiyunani. Kutozimia roho – kujiingiza katika uovu, kukosa ujasiri.

Imani ya Paulo ilikuwa na nguvu.

Ebu na tuangalie baadhi ya sababu zilizofanya akawa na nguvu.

Kumbuka Bwana yu pamoja nawe

Katika sehemu ya kwanza ya kifungu hiki Paulo alitoa baadhi ya sababu ni kwa nini alikuwa na ujasiri. Tazama hizi:

Ulinganifu wake unaonyesha kwamba Mungu alikuwa pamoja naye.

2 Kor. 4:8-9, "*Pande zote twadhikika, bali hatusongwi; twaona shaka bali hatukati tamaa; twaudhiwa, bali haatuachwi; twatupwa chini, bali hatuangamizwi;*"

Bwana alimsaidia katika kila aina ya ugumu aliokumbana nao.

Alishikilia imani yenye nguvu.

2 Kor. 4:13, "*Lakini kwa kuwa tuna roho ile ile ya imani; kama ilivyoandikwa, Naliamini na kwa sababu hiyo nalinena; sisi nasi twaamini, na kwa sababu hiyo twanena;*"

Alishikilia imani yenye nguvu katika neno la Mungu na akaifundisha kwa upole.

Aliamini katika ufufo. 2 Kor. 4:14, "*Tukijua ya kuwa yeye aliyemfufua Bwana Yesu atatufufua sisi nasi pamoja na Yesu, na kutuhudhurisha pamoja nanyi.*"

Na aliamini kwamba ssisi sote tutafufuliwa siku moja.

Alifurahia mazuri aliyokuwa anafanya.

2 Kor. 4:15, "*Kwa maana mambo yote ni kwa ajili yenu, ili neema hiyo ikiongezwa sana, kwa hao walio wengi shukrani izidishwe, na Mungu atukuzwe.*"

Siyo kwamba anapaswa kujisifu, lakini kwamba wengine waweze kuwa na faida kwa kuhubiri kwake neno la Mungu; alimpa Mungu utukufu kwa kukubali kwao neno lake maana alijua kwamba Bwana alikuwa pamoja naye alipokuwa anahubiri.

Mat. 18:20, "*Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, mimi nipo papo hapo katikati yao.*"

Kumbuka utu wa ndani ulikuwa ukifanywa upya siku baada ya siku

2 Kor. 4:16, "*Kwa hiyo hatulegei; bali ijapokuwa utu wetu wan je unachakaa, lakini utu wetu wa ndani unafanywa upya siku kwa siku.*"

Utu wake wan je ulikuwa unaharibika.

Kuna mfumo wa uzee wa kiasili katika miili yetu. Kulikuwa na kusinyaa kwa mwili kwa sababu ya mateso, hofu, na matatizo.

- 1 Pet. 1:24, "*Maana mwili wote ni kama majani, na fahari yake yote ni kama ua la majani. Majani hukauka na ua lake huanguka.*"
- Yakobo 4:14, "*Walakini hamji yatakayokuwako kesho. Uzima wenu ni nini? Maana ninyi ni mvuke uonekanao kwa kitambo, kisha hutoweka.*"
- Ayubu 29:18, "*Ndipo nikasema nitakufa ndani ya kioto change, nami nitaziongeza siku zangu kama mchanga;*"

Ayubu alingalia mbele kwa wakati ambao angekuwa na Bwana wake na kuishi milele mbinguni.

Utu wa ndani ulikuwa unafanywa upya.

Utu wa ndani ni roho au nafsi. (Utu uliojificha wa mwanadamu).

1 Pet. 3:4, "*Bali kuwe utu wa moyoni usioonekana , katika mapambo yasiyoharibika; yaani roho ya upole na utulivu, iliyo ya thamani kuu mbele za Mungu.*"

Angalia roho zetu:

Roho inajua, hutafakari, hufikiria. 1 Kor. 2:11, "*Maana ni nani katika binadamu ajuaye mambo ya binadamu ila roho ya binadamu iliyo ndani yake?...*"

Roho inarudi kwa Mungu aliyeitoa. Mhu. 12:7, "*Nayo mavumbi kuirudia nchi kama yalivyokuwa, nayo roho kumrudia Mungu aliyeitoa.*"

Inafanywaje upya?

Kwa kufanya karamu katika neno la Mungu.

- 1 Pet. 2:2, "*Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu.*"
- 2 Pet. 3:18, "*Lakini kueni katika neema, na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo. Utukufu una yeye sasa na hata milele.*"

Roho zetu pia hufanywa upya tunaposhiriki meza ya Bwana.

Kumbuka kuzingatia matatizo kama "kujikwaa kwepesi" kulinganisha na uzima wa milele

2 Kor. 4:17, "*Maana dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana.*"

Angalia maandiko haya yanaendana na somo hili.

2 Tim. 2:12, "*Kama tukistahimili, tutamiliki pamoja naye; kama tukimkana yeye, yeye naye atatukana sisi;*"

Hakika paulo aliteseka katika huduma yake kwa Kristo.

- 1 Pet. 4:13, "*Mkilaumiwa kwa ajili ya jina la Kristo ni heri yenu; kwa kuwa Roho wa utukufu na wa Mungu anawakalia.*"
- Rum. 8:17, "*Na kama tu watoto, basi tu warithi; warithi wa Mungu, warithio pamoja na Kristo; naam, tukiteswa pamoja naye ili tupate na kutukuzwa pamoja naye.*"

Angalia baadhi ya mateso ya Paulo ambayo alichukulia kama nyepesi.

2 Kor. 11:22-28, "*Wao ni Waebrania? Na mimi pia, wao ni uzao wa Ibrahimu? Na mimi pia. Wao ni wahudumu wa Kristo? (Nanena kiwazimu), mimi ni zaidi; katika taabu kuzidi sana; katika kifungo kuzidi sana; katika mapigo kupita kiasi; katika mauti mara nyingi. Kwa Wayahudi mara tano nalipata mapigo arobaini kasoro moja. Mara tatu nalipigwa na bakora; mara moja nalipigwa kwa mawe, mara tatu nalivunjikiwa jahazi; kuchwa kucha nimepata kukaa kilindini; katika kusafiri mara nyingi; hatari za mito; hatari za wanyang'anyi; hatari kwa taifa langu; hatari kwa mataifa mengine; hatari za mjini; hatari za jangwani; hatari za baharini; hatari kwa ndugu za uongo; katika taabu na masumgufu; katika kukesha mara nyingi; katika njaa na kiu; katika kufunga mara nyingi; katika baridi na kuwa uchi. Baghairi ya mambo ya nje, yako yanijiayo kila siku, ndiyo maangalizi ya makanisa yote.*"

Paulo alichukilia mateso haya kirahisi kama yanavyolinganishwa na mbingu na uzima wa milele.

Petro aliandikwa kwamba ni furaha isiyokifani – utukufu wa mbinguni ni mzuri zaidi ya aina yoyote ya mateso hapa duniani. Ndiyo maana Paulo akaichukulia rahisi.

Paulo aliandika uzito wa utukufu – Gk. Kuwa na uzito mkuu. Katika ulinganifu, mbingu ina vitu vingi vizuri zaidi na furaha, kuliko maumivu ya mateso. Mtu anaweza kudhani kwamba wakati maumivu yanakuwa mazito. Haiwi katika mtazamo wa ulinganifu wa furaha ya mbingu.

Kumbuka kuangalia vitu visivyoonekana

2 Kor. 4:18, "*Tusiviangalie vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Kwa maana vinavyoonekana ni vya muda tu; bali visivyoonekana ni vya milele.*"

Vitu vinavyoonekana – Gk. Muda mfupi, kwa sababu.

Hii inajumuisha mateso.

Hii inajumuisha vitu vinavyovutia tamaa ya mwili.

1 Yohana 2:15-16, "*Msiipende dunia wala mambo yaliyomo katika dunia, mtu akiipenda dunia kumpenda Baba hakumo ndani yake. Maana kilaa kilichomo duniani, yaani tama ya mwili, tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia.*"

Vitu visivyoonekana.

Hizi ni vya kiroho, vitu vya milele. Inajumuisha vitu ambavyo husaidia kuipa nafsi nguvu.

Mwandishi wa Waebrania alishikilia kauli hii kiroho.

- Heb. 11:1, "*Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.*"
- Heb.11:3, "*Kwa imani twafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyodhahiri.*"
- Heb. 11:7, "*Kwa imani Nuhu akiisha kuonywa na Mungu katika habari za mambo yasiyoonekana bado, kwa jinsi alivyomcha Mungu, aliunda safina apate kuokoa nyumba yake. Na hivyo akauhukumu makosa ulimwengu, akawa mrithi wa haki ipatikanayo kwa imani.*"

Hatuitazamii mbingu kama bado, lakini tunajua kwa imani kwamba ipo maana Bwana ametuambia hivyo.

Hitimisho

Mambo haya ambayo Paulo anataja inatuweka wazi sisi kama Wakristo.

Huduma zote ambazo Mungu anatuambia tufanye, kila mzigo aliotubebesha, kila ugumu tunaoushinda imekusudiwa kwa ajili ya mazuri yetu; na, ikipokewa katika roho ya utii na wanawaamifu, tutafurahia utajiri wa baraka ambayo Mungu ametutunzia kwao wampendao.

Usiseme mzigo wa Bwana.

Yer. 23:33-40, "*Na watu hawa au nabii au kuhani atakapokuuliza, akisema mzigo wa BWANA ni nini? Ndipo utawaambia mzigo gani? BWANA asema nitawatupilia mbali. Na katika habari ya nabii, na kuhani, na watu, watakaosema, mzigo wa BWANA, mimi nitamwadhibu mtu yule, na nyumba yake. Mtasema hivi kila mtu na jirani yake, na kila mtu na ndugu yake, BWANA amejibu mtu? Na BWANA amesemaje? Na mzigo wa BWANA hamtautaja tena; maana neno la kila mtu ndilo litakaalo kuwa mzigo wake; maana ninyi mmeyapotosha maneno ya Mungu aliyehai, ya BWANA wa majeshi, Mungu wetu. Nawe utamwambia nabii hivi, BWANA amekujibu nini? Na BWANA amesemaje? Lakini akisema mzigo wa BWANA, basi, BWANA asema hivi, kwa sababu mwasema neno huli; mzigo wa BWANA; nami nimemtuma mtu kwenu kusema, msiseme mzigo wa BWANA; basi kwa hiyo angalieni nisije nitawasahau ninyi kabisa, nami nitawatupilia mbali, pamoja na mji huu niliowapa ninyi na baba zenu, mtoke mbele ya uso wangu; nami nitaleta juu yenu aibu ya milele, na fedheha ya daima ambayo haitasahauliwa.*"

Mkristo anayekataa wajibu wake na kuruka majukumu yake atajikuta hafai kwa ajili ya heshima na utukufu ambao Mungu amewatunzia watumishi wake waaminifu.